



TANGAZO KWA UMMA

KUFUTWA KWA LESENI YA KUFANYA BIASHARA YA KIBENKI YA MBINGA COMMUNITY BANK NA KUWEKWA CHINI YA UFLISI

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 56(1)(g), 56(2) (a), (b) na (d), 58(2)(i), 11(3)(j), 61(1) na 41(a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeamua kuifunga Mbinga Community Bank Plc; kusitisha shughuli zake zote za kibenki; kufuta leseni yake ya biashara ya kibenki; kuiweka chini ya ufilisi; na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board) kama mfilisi kuanzia tarehe 12 Mei, 2017.

Uamuzi huu umechukuliwa baada ya Benki Kuu ya Tanzania kujiridhisha kuwa Mbinga Community Bank Plc ina upungufu mkubwa wa mtaji na ukwasi kinyume na matakwa ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huu wa mtaji na ukwasi unahatarisha usalama wa sekta ya fedha, na kwamba kuendelea kwake kutoa huduma za kibenki kunahatarisha usalama wa amana za wateja.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenyewe amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya fedha.

BENKI KUU YA TANZANIA

12 Mei, 2017